

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAMISEMI

PRIMARY EDUCATION SERVICES NETWORKING ORGANIZATION (PESNO)



SIMU: 0713- 526533

0767- 526533

MTIHANI WA ZIADA WA UTAMILIFU KWA DARASA LA SABA

SOMO: SAYANSI [03]

MUDA: SAA 1:30

JINA LA MTAHINIWA: _____


JINA LA SHULE: _____

WILAYA: _____ **MKOA:** _____

MAELEKEZO:

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya majibu
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. chagua jibu sahihi kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia (OMR) kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya karatasi ya (OMR)
5. Hakikisha kazi yako iko nadhifu na safi
6. Mtihani huu una kurasa nne zilizochapishwa

Katika swali la 1-40 chagua jibu sahihi kisha weka kivuli katika herufi ya jibu hilo katika fomu ya jujibia

1. Wanakijiji wa Ulima wanakula vyakula vifuatavyo; wali, nyama, samaki na maboga. Ili kupata chakula bora inabidi waongeze chakula gani?
a. Mayai na mbogamboga b. karanga na mbogamboga c. matunda na parachichi
d. mihogo na karoti e. matunda na mbogamboga
 2. Mmea una sehemu kuu ngapi?
a. Mbili b. moja c. nne d. tano e. tatu
 3. Ni kioo gani tunaweza kutumia ili taswira zetu zionekane vizuri?
a. Mbonyeo b. bapa c. mbinuko d. lenzi e. prizimu
 4. Seli zipi kati ya zifuatazo hudumu kwa muda wa miezi minne?
a. Nyekundu b. pazima c. nyeupe d. sahani e. nyekundu na nyeupe
 5. Ni aina gani ya chakula ambacho mmeng'enywa wake huanzia sehemu iliyooneshwa kwa herufi V?
a. Wanga
b. Fati na Mafuta
c. Protini
d. Vitamini
e. Madini na chumvi
- 
6. Mbegu hutawanywa kwa njia mbalimbali; nazi hutawanywa kwa njia ya –
A maji b. upepo c. jua d. kupasuka e. hewa
 7. Zifuatazo ni njia zinazotumika katika kutunza na kutumia dawa **ISIPOKUWA**
a. Dawa zihifadhiwe mbali na Watoto
b. Dawa zilizopitwa na wakati zinaweza kutumika ila kwa maelekezo ya daktari
c. Kila dawa ibandikwe jina na maelekezo namna ya kutumia
d. Dawa zitumike kufuata maelekezo ya daktari
e. Nawa mikono kwa sabuni baada ya kutumia dawa
 8. Baadhi ya bakteria hurutubisha ardhi kwa-
a. Kuoza vitu b. kupunguza ukuaji wa wadudu c. kuharibu magugu
d. kuongeza kiasi cha oksijeni e. kuongeza joto ardhi
 9. Ugonjwa wa matende huenezwa na mdudu anayeitwa-
a. Mbung'o b. inzi c. mende d. kiroboti e. mbu
 10. Yapi kati ya magonjwa yafuatayo husababishwa na virusi?
a. Pepopunda, kifua kikuu na surua b. surua, kifaduro na tetekuwanga c. tetekuwanga, kichocho na kipindupindu d. kipindupindu, polio na surua e. polio, tetekuwanga na surua

11. Alama  huwakilisha kifaa kinachotumika kupima-

- a. mkondo wa umeme b. ukinzani c. uwepo wa umeme katika sakiti
d. kani ya msukumo wa umeme e. transfoma


12. Vipi kati ya vitu vifuatavyo haviwezi kuakisi sauti?

- a. Ukuta b. sofa na sponji c. ukuta mfupi d. nyumba kubwa e. milima mirefu

13. Sauti inaweza kusafiri katika maada zifuatazo **ISIPOKUWA-**

- a. Chuma b. maji c. vakyumu d. uzi e. hewa

14. Mchoro huu huwakilisha kifaa kinachotumika:



- a. Kuangalia vitu vya mbali kama angani
b. Kuangalia vitu vidogo kama bakteria
c. Kuangalia vitu vilivyojificha mfano nyuma ya mlima
d. Kupima urefu wa vitu kama meza
e. kupima uzito wa kitu kama mchele

15. Sehemu kubwa ya mfumo wa fahamu unatawaliwa na;

- a. Milango ya fahamu b. mishipa ya damu c. uti wa mgongo d. ubongo e. neva

16. Kutokwa na damu kwenye fizi za meno na vidonda kuchelewa kupona hutokana na ukosefu wa vitamini gani? a. K b. E c. B₂ d. C e. A

17. Kufanya mazoezi mara kwa mara inaweza kuwa suluhisho kwa tatizo lifuatalo;

- a. Kwashakoo b. shinikizo la juu la damu c. shinikizo la chini la damu
d. upungufu wa damu e. utapiamulo

18. Mkasi ni mfano wa nyenzo daraja la:

- a. Pili b. kwanza c. tatu d. sita e. tano

19. Ipi kati ya ogani zifuatazo haizalishi homoni?

- a. Kongosho b. ovari c. ini d. korodani e. kuta za tumbo


20. Ipi kati ya hizi ni dalili ya kisonono?

- a. Kuwasha sehemu za siri b. kukojoa mara chache c. kutokwa na usaha na maumivu makali wakati wa kukojoa
d. kutokwa na damu kwenye njia ya mkojo e. upele sehemu za siri

21. Uwiano kati ya kani ya mzigo na kani ya egemeao(jitihada) huitwa—

- a. Manufaa ya kimakanika b. kanuni ya mwendo c. mwendokasi d. mwendo Dhahiri
e. wenzo

22. Tafuta thamani ya X katika mchoro ufuatao



- a. Sm 8 b. sm 2 c. sm 16 d. sm 4 e. sm 10

23. Ili kuzuia upungufu wa damu, mama mjamzito anatakiwa kupata lishe yenye

- a. Chumvichumvi b. wanga c. protini d. vitamini e. fati

24. Binadamu kamili ana mbavu ngapi?

- a. 12 b. 10 c. 20 d. 25 e. 24

25. Ni kipimo kipi kati ya hivi hutumika kupima kiwango cha unyevunyevu katika hewa?

- a. Barometa b. anemometa c. thermometa d. haigrometa e. periskopu

26. Sehemu ya ua ambayo ina rangi ya kijani huitwa-

- a. Petali b. sepali c. stigima d. ovari e. filament

27. Mmea hupoteza maji kwa njia gani?

- a. Translokesheni b. transpiresheni c. respiresheni d. fotosinthesisi e. osmosis

28. Adui mkubwa wa virusi vinavyosababisha ukimwi mwilini ni-

- a. Moyo b. ARV c. seli hai nyeupe d. plazima e. seli nyekundu za damu

29. Nini wajibu wa jamii kwa watu wanaoishi na VVU?

- a. Kuwatibu kwa kutumia dawa za VVU b. kuwatenga na watu wengine c. kula au kucheza nao kwa tahadhari d. kuwapenda, kuwasaidia na kuwashauri e. kuwakusanya sehemu moja ili kuwasaidia

30. Mtu mwenye VVU anaweza kutambuliwa kwa;

- a. Mwonekano b. mahudhurio hospitalini c. tabia zake d. kukohoa sana e. kupima damu

31. Ili tendo la osmosis lifanikiwe, kunahitajika kuwepo na

- a. Kiazi, maji na jiwe b. kiasi, maji na chumvi c. kiasi bila kitu kingine d. kiasi, kisu na jiwe e. kiasi, maji na mchanga

32. Mapacha wa kufanana kwa kila hali hutokana na

- a. Yai moja lililogawanyika mara mbili b. yai moja ambalo halijagawanyika c. mayai mawili ambayo hutokana na ovari moja d. mayai mawili ambayo hayakugawanyika e. yai moja yenye viini viwili

33. Kipi ni kitendo ambacho si utoaji wa taka mwilini?

- a. Utoaji wa kabondayoksaidi b. utoaji wa jasho c. kukojoa d. utoaji kinyesi e. utoaji chumvichumvi

34. Huduma ya kwanza hutolewa na –

- a. Matabibu b. polisi c. vikosi maalum d. mtu mwenye ujuzi e. nesi tu

35. Ili uweze kugomboa chumvi kutoka kwenye maji; njia ipi inafaa?

- a. Kuvukiza b. kutenganisha c. kuchemsha d. kutumia karatasi ya rangi e. kuchuja

36. Hatua ya nne katika utafiti wa kisayansi ni-

- a. Hitimisho b. dhanio c. kukusanya data d. kugundua tatizo e. uchambuzi wa data

37. Umeme una uhusiano na –

- a. mwanga b. chuma c. upepo d. joto e. sumaku

38. Vifuko vidogovidogo vilivyomo ndani ya mapafu huitwa

- a. Bronchioli b. viribahewa c. daiframu d. fumbatio e. umio

39. Yupi kati ya Wanyama wafuatao hana uti wa mgongo?

- a. Nyoka b. jongoo c. njiwa d. chura e. kunguru

40. Metali ambayo ipo katika hali ya kimiminika ambayo hutumika kwenye kipimajoto ni-

- a. Magneziamu b. aluminiamu c. kalisiamu d. sodiamu e. zebaki

SEHEMU B: MAJUBU MAFUPI

41. Gesi gani hutumika na miemea aina ya mikunde kurutubisha ardhi?

42. Taja njia moja ambayo hutumika kuhifadhi au kutunza data za uchunguzi wa kisayansi.

43. Hakuna mashine yenye ufanisi wa 100%. Kani gani husababisha kupotea kwa ufanisi huo?

44. Ogani gani mwilini ina nguvu sana na hutumika kusukuma damu?

45. Tafuta thamani ya R_1 wakati swichi ikiwa imefungwa

